ST. PETER CLAVER HIGH SCHOOL
P.O Box 2175 Dodoma, Tanzania
Tel: (+255) 0653 738 060; 0759933067
Website www.stpeterclaver.ac.tz; Email: jamesyawa@yahoo.com
To Learn To Love To Serve

MAHITAJI YA MWANAFUNZI KUJIUNGA KIDATO CHA TANO 2020/2021

Vyote vyenye * vinapatikana shuleni.

1. **TRANKA:** tranka moja kwa ajili ya nguo, madaftari na vitabu. Mabegi ya aina nyingine hairuhusiwi.
2. ***BEGI LA MGONGONI JEUSI:** Moja kwaajili ya kubeba vitu vidogo vidogo. Aina nyingine za begi dogo haziruhusiwi.
3. ***MASWETA YA SHULE:** yawe mawili yanapatakana duka la shule. Masweta ya aina nyingne hayataruhusiwi.
4. ***VIZIBAO:** (masweta bila mikono) 2. Vinapatikana duka la shule, Vya aina nyingine haviruhusiwi.
5. ***KOTI NA TAI:** kwa ajili ya baridi litapatikana shuleni. Aina nyingine ya koti au tai havitaruhusiwa.
6. ***SURUALI / SKETI ZA DARASANI**: Pea 2 za suruali rangi ya kijivu (kwa mvulana) na sketi 2 za blue (kwa msichana). Suruali na sketi zinazoruhusiwa ni zile tu zinazouzwa kwenye duka la shule.
    - Haziruhusiwi kubana suruali (modo),au kuvaa “mlegezo” mzunguko wa chini wa suruali unatakiwa usipungue upana wa inchi 18.
    - Hairuhusiwi sketi ambayo ni fupi. Sketi inapaswa kuwa angalau inchi 12 kutoka kwenye unyayo au soli ya viatu, mbele na nyuma.
7. ***SURUALI / SKETI ZA KUSHINDIA**: Pea 2 za suruali rangi ya maroon (kama mwanafunzi ni mvulana) na sketi 2 maroon (kwa msichana). Suruali na sketi zinazoruhusiwa ni zile zinazouzwa kwenye duka la shule tu.
    - Haziruhusiwi suruali zinazovaliwa kwenye “mlegezo” ama zinazobanwa(modo): mzunguko wa chini wa suruali unatakiwa usipungue upana wa inchi 18.
    - Hairuhusiwi sketi ambayo ni fupi. Sketi inapaswa kuwa angalau inchi 12 kutoka kwenye unyayo au soli ya vyatu, mbele na nyuma.
8. ***T.SHIRTS 3 ZA KUSHINDIA:** zenye nembo ya shule na zinapatikana shuleni tu.
   N.B.: T-shirts za rangi nyingine, hata nyeupe, haziruhusiwi. Pia haziruhusiwi t-shirts zinazobanwa ama zilizokatwa mikono.
9. ***NGUO YA MICHEZO 1:** itavaliwa wakati wa michezo na ni lazima iwe na nembo ya shule. Nguo zote za michezo zinapatikana shuleni na zinavaliwa kwenye muda wa michezo tu.
10. ***TRACK-SUITS:** zinapatikana duka la shule, zisiwe zimebanwa na pia, katika kuvaliwa, zisivaliwe zikiwa zimekunjwa magotini. Track- suit itavaliwa kwa ajili ya kujihifadhi na baridi wakati wa kujisomea usiku.
11. ***MASHUKA 2 NA FORONYA:** yanapatikana shuleni.
12. **BLANKETI 1.**
13. **MATAULO 2:**
14. **KANDAMBILI KWA** ajili ya bafuni tu, Ziwe za kawaida kabisa (mtindo wa Bata), bila marembo.
15. **VIATU VYEUSI** vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kamba jozi 2.
16. ***SOKSI ZA DARASANI:** nyeupe ndefu (Free size) jozi 4. Haziruhusiwi soksi fupi za aina yoyote ile yanye urembo au maandishi aina yeyote.
17. **RABA:** jozi moja (1) za michezo. Viatu ama raba za michezo ziwe zenye kamba na nyeupe tu na zisiwe zimeandikwa maandika aina yeyote si za aina nyingine mbadala. Wanafunzi wanaocheza mpira wa miguu au mpira wa kikapu wanaruhusiwa kuwa na jozi nyingine ya raba (six) za pekee kwa ajili ya michezo hiyo.
18. ***SOKSI ZA MICHEZO:** jozi 1 zenye nembo ya shule zinazopatikana shuleni.
19. **VIATU VYA WAZI / SANDALS:** viwe vyenye mikanda miwili mbele na si ya mtindo wa kandambili. Rangi yake iwe nyeusi ama rangi ya udongo. Vinaruhusiwa kuvaliwa usiku wakati wa kujisomea tu au jumamosi na jumapili mchana. Mifano ya sandals zinazotakiwa
    (si lazima ziwe hizo hizo lakini mtindo uwe huu pembeni kwenye picha)

20. **NGUO ZA NDANI** za kutosha yaani: Chupi kwa wasichana Skintite na Underskirt/andasketi, Vesti vinaruhusiwa kwa ajili tu ya kuvaliwa ndani ya shati nyeupe za shule. Ziwe vesti za kawaida kabisa bila urembo au maandishi yeyote. **N.B.: Nguo za ndani zote ziwe nyeupe tu hatuhitaji rangi nyingine**!
21. **NGUO YA USIKU (NIGHT-DRESS) 1 AU 2:** ziwe za heshima
22. **KHANGA/KITENGE** doti moja (kwa wasichana). Zivaliwe bwenini tu.
23. **SAA YA MKONONI**. Isiwe kubwa na iwe ya rangi **NYEUSI TU**.
24. **MKANDA 1 MWEUSI WA NGOZI**: kwa wavulana tu, kwa ajili ya kuvaa kwenye suruali zao. Uwe wa kawaida kabisa, bila urembo na bakoni (sehemu ya kufungia) isiwe kubwa.
25. ***VYOMBO VYA CHAKULA**: sahani 1, kijiko 1, kikombe 1 na chupa kwa ajili ya maji 1 ya kunywa. Zinapatikana shuleni tu.
26. ***NDOO YA PLASTIKI** moja ya lita 20. Inapatikana shuleni.
27. Madaftari makubwa yasiopungua 15 (Counter books quire 3)

28. Tochi ya batri 1
29. Kufuli ndogo 2
30. Karatasi za kuandikia barua pamoja na stampu zisizozidi tano kwa muhula
31. Box file 2 (kwa ajili ya kuhifadhia mitihani)
32. Biblia 1
33. Kamusi ya kiingereza 1 na kamusi ya Kiswahili 1
34. Mto wa kulalia 1 kama anatumia

- ***MAHITAJI MENGINE:** mafuta ya kujipaka, dawa ya meno, mswaki, toilet papers, dawa ya viatu (kiwi), sabuni za kuogea na kufulia za kutosha, Vitambaa vya mikononi vinne (handkerchiefs)
- Kitana cha kuchania nywele, henga za kutundikia nguo 6, Jozi moja ya vibanio vya kuanikia nguo. Vitu hivi vyote vinapatikana pia kwenye duka la shule, Pia unaruhusiwa kuja navyo kutoka nyumbani ila sababu ni vitu vya kuisha mtoto akatapomaliza vitu hivyo atanunua duka la shule na sio kupiga simu nyumbani kuletewa.

N.B.:

- Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani siku ya kureport, afike shuleni akiwa amevaa sare kamili ya shule (*full school uniform).*
- Kila nguo (hata za ndani) inapaswa kua na alama inayomtambulisha mwanafunzi, yaani jina lake. Jina hilo linapaswa kufumwa au kuchapishwa pale tu ambapo wanafunzi wameambiwa lifumwe au kuchapishwa. Haliruhusiwi kuandikwa na peni na pia linapaswa kuwa kubwa kiasi.
- Haziruhusiwi dawa za kienyeji. Dawa zote zinapaswa kuonyeshwa kwa nesi wa shule.
- Haziruhusiwi marashi na vipodozi vya aina yoyote, pamoja na rangi ya kucha, rangi ya midomo, lip-balm, lip-stick, angel face, parfume, deodorant, spray n.k.
- Haviruhusiwi vitu visivyosaidia masomo yao au visivyo na maana katika mazingira ya shule, kama vile:
  - bangili, pete, hereni culture na urembo wa aina nyingine zote;
  - “diary” au agenda za binafsi; picha au album za picha;
  - vidoli;
  - cds na albums za muziki:
  - flash, ipad
  - camera,
  - simu za mikononi (hata kwa wanafunzi wanaotoka sehemu yeyote nje ya mkoa wa Dodoma).

Asanteni kwa kuzingatia yote yaliyoandikwa hapo juu. Tunaomba sana mwanafunzi asije na kitu chochote kile ambacho hakijaandikwa katika orodha hiyo. Asanteni na karibuni **St. Peter Claver High School.**

ST. PETER CLAVER HIGH SCHOOL
P.O Box 2175 Dodoma, Tanzania
Tel: (+255) 0653 738 060; 0759933067
Website: www.stpeterclaver.ac.tz; Email: spclaverhs@gmail.com
To Learn To Love To Serve

Form NO. 2 A 3

Mahitaji siku ya Kufungua shule Kidato Cha kwanza 2020

S/N	MAHITAJI YA MWANAFUNZI (Mahitaji yenye nyota yanapatikana shule na bei zake)	IDADI	BEI KILA MOJA	KWA MATUMIZI YA OFISI TU
1.	Risiti ya malipo ya Ada			
2.	Risiti ya Malipo ya Pocket money / transport			
3.	Tranka	1		
4.	Begi la mgongoni jeusi	1		
5.	Masweta ya shule **,	2	30,000/-	
6.	Vizibao vya shule **	2	30,000/-	
7.	Koti la Shule na tai **	1	50,000/-	
8.	Shirt la shule **	2	20,000/-	
9.	Skirt ya shule**	2	30,000/-	
10.	Skirt ya kushindia **	2	30,000/-	
11.	Suruali Za Shule **	2	30,000/-	
12.	Suruali za Kushindia **	2	30,000/-	
13.	T – shirt za Shule **	2	15,000/-	
14.	T- shirt ya kushindia **	1	15,000/-	
15.	Track suit ya shule **	1	35,000/-	
16.	Mashuka na Foronya **	1	35,000/-	
17.	Blacket	1		
18.	Mataulo	2		
19.	Viatu vya Shule Vyeusi Vya kamba	2		
20.	Soski Nyeupe za darasani **	4	3,000/-	
21.	Raba za Michezo Nyeupe	1		
22.	Nguo za Michezo **	1	30,000/-	
23.	Viatu vya Wazi (sandals tazama Mfano juu fomu ya kwanza)	1		
24.	Nguo za ndani: NB: wasichana ni nyeupe tu	Za Kutosha		
25.	Nguo ya Kulalia (nignt Dress)	1		
26.	Khanga /Kitenge (kwa wasichana tu)	Doti 1		
27.	Saa ya mkononi yenye mkanda mweusi tu	1		
28.	Mkanda (Wavulana tu Usio na Bakoni wala Urembo wowote)	2		
29.	Sahani, Kikombe na Kijiko (serving Dishes)**	1	12,000/-	
30.	Chupa ya maji ya kunywa **	1	10,000/-	
31.	Mafuta ya kujipaka isiwe lotion ya kunukia sana	Kopo 2		
32.	Dawa za Meno Kubwa	Tube 1		
33.	Miswaki imara	2		
34.	Ndala zisizo na Urembo wowote (Bata)	Jozi 1		
35.	Toilet Paper	Dozen 1		
36.	Dawa ya Viatu (Kopo Kubwa)	Kopo 2		
37.	Sabuni za kuogea	Dozeni 1		
38.	Sabuni za Kufulia	Kilo 5		
39.	Suit	1	75,000/=	

******FOMU HII NI MALI YA SHULE TAFADHALI NJOO NAYO KATIKA UKAGUZI SIKU YA KUFUNGUA SHULE******

Jina la Mkaguzi **Idara** **Sahihi** **Tarehe**

_____ _____ _____ _____